Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 8 Aprili, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## WIMBO WA TAIFA

*(Hapa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## KIAPO CHA UAMINIFU

Wajumbe wafuatao waliapa Kiapo cha Uaminifu na kukaa katika nafasi zao Bungeni:-

Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro
Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ungetulia kwanza tafadhali ili tukio hili lipite**.**

*(Hapa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani walitoka Ukumbini)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo asubuhi Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, alinifuata nyumbani na kunieleza kwamba, kabla ya kipindi cha maswali na majibu, Wabunge wa Kambi ya Upinzani wote watatoka nje ya Ukumbi, wakipinga wanachodai wao kwamba ni kusuasua kwa mazungumzo kuhusu Muafaka wa Zanzibar. *(Kicheko)*

## T A A R I F A  Y A  S P I K A

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijatoa taarifa, kwa niaba yenu, ningependa niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wawili wapya, ambao nimewaapisha sasa hivi Bungeni; Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro na Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir, karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, ninafurahi kutoa taarifa kwamba, Mheshimiwa Rais amekwisha kutoa kibali na kuweka sahihi kukubali Miswaada ifuatayo, ambayo

tuliipitisha katika Mkutano wa Kumi; Miswada hiyo ni *The National Prosecution Service Act, 2008* unakuwa sasa Na. 27 wa 2008; *The HIV/AIDS, Prevention and Control Act, 2008* unakuwa Na. 28 wa 2008; na *The Tourism Act*, *2008* unakuwa Na. 29 wa 2008.

**HATI ILIYOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU, URATIBU, SERA NA BUNGE:**

Taarifa ya Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 1

**Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu *(CDA)***

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu *(CDA)* ndiyo yenye jukumu la kupima viwanja, kusanifu michoro na barabara katika Manispaa ya Dodoma: Je, ni lini *CDA* itapewa uwezo kifedha ili kusanifu barabara katika maeneo mapya ya *Area E,* Ipagala, Kisasa, Nzuguni na kadhalika ndani ya Manispaa ya Dodoma?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Felister Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Baada ya maamuzi ya mwaka 1973 ya kuhamisha Makao Makuu ya nchi kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma, Serikali ilitayarisha mpango kabambe wa uendeshaji Mji Mkuu, ambao uliidhinishwa mwaka 1976. Katika utekelezaji wa mpango wa miaka mitano ya kwanza, huduma kuu za msingi *(Dodoma Trunk Service - DTS)* zilizobuniwa zilikuwa zitekelezwe kwa awamu tatu. Katika mpango huo uliowezeshwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)*, zilitekelezwa awamu mbili tu zilizokamilika mwaka 1987. Awamu ya tatu haikutekelezwa kutokana na ukosefu wa fedha. Ili kuendelea kutekeleza mpango kabambe, Serikali imeendelea kuitengea Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu fedha kwa ajili ya kuendeleza Mji wa Dodoma kama ifuatavyo:-

(i) Katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, Serikali iliitengea *CDA* shilingi 105,000,000, kwa ajili ya usanifu wa miundombinu katika eneo la *Area A*, lenye wakazi

wengi lakini halina miundombinu. Tayari mtaalamu mshauri wa kufanya usanifu wa miundombinu ya eneo hilo, ameteuliwa kwa njia ya tenda.

(ii) Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Serikali iliitengea *CDA* shilingi 450,000,000 kwa ajili ya usanifu wa miundombinu katika eneo la *Area E* na shilingi 350,000,000 kwa ajili ya kufungua barabara chache, ziweze angalau kupitia katika baadhi ya maeneo. *CDA* inakusudia kutumia kiasi hicho kwa kujenga kilomita tano za barabara kwa kiwango cha changarawe, ikijumuisha mifereji ya maji ya mvua na madaraja katika eneo la Kisasa. Mkandarasi wa kufanya kazi hizi ameshapatikana kwa njia ya tenda. Aidha, mchakato wa kumpata mtaalamu mshauri kwa ajili ya usanifu wa miundombinu katika eneo la *Area E* bado unaendelea kwani mpaka sasa mamlaka imetangaza na kupokea *expression of interest* kwa kazi hiyo kutoka makampuni mbalimbali.

(iii) Katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Serikali inatarajia kuitengea *CDA* kiasi cha shilingi 3,850,000,000 kwa ajili ya kuendeleza miundombinu katika maeneo mbalimbali ya Mji wa Dodoma. Fedha hizo zinatarajiwa kujenga km sita za lami katika eneo la *Area A*, km tano za changarawe katika eneo la Ipagala na km tano za changarawe katika eneo la uboreshaji la Chang'ombe.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza tena swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali ilikuwa na Mpango Kabambe kwa awamu tatu kuuendeleza Mji wa Dodoma kupitia Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu; je, ni lini Serikali itatimiza Mpango Kabambe wa awamu ya tatu wa kuiendeleza Manispaa ya Dodoma kwa sababu hatua alizozieleza ni hatua za awamu na wala siyo Mpango Kabambe ambao ulipangwa na Serikali?

Swali la pili; je, Serikali itakubaliana nami kwamba, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu hawana vitendea kazi vya kutosha, ndiyo maana ustawishaji Makao Makuu unakwenda kwa mwendo wa kusuasua?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, ninapenda kumjibu Mheshimiwa Felister A. Bura, maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza, kama nilivyoelezea katika jibu la msingi nilielezea kwamba, Mpango Kabambe ulitekelezwa hadi mwaka 1987. Sote tukumbuke kwamba, baada ya 1987 katika nchi yetu kulitokea nini; kulikuwa na vita dhidi ya Idd Amin na hivyo bajeti ya nchi ilipungukiwa fedha, ndiyo maana mpango huu ulisimama hadi miaka ya karibuni na ndiyo maana sasa hivi tunaitengea *CDA* fedha nyingi zaidi za maendeleo. Hii ni ishara kwamba, awamu ya tatu juu ya Mpango Kabambe unaanza kutekelezwa.

Pili, kwa upande wa watumishi wa *CDA* kutokuwa na vitendea kazi, ninapenda kusema kwamba, pamoja na kwamba Serikali inaiongezea Bajeti *CDA*, lakini pia Uongozi wa *CDA* unajitahidi iwezekanavyo, kuziba mianya mbalimbali, ambayo fedha zilikuwa zinapotea na fedha hizi hatimaye zitasaidia kuongeza vitendea kazi.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Ninashukuru Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa inaonekana wazi kwamba, hakuna mkazo maalumu wa kuweza kuujenga Mji wa Dodoma kutoka kwa Serikali na hata ukitazama miundombinu kama vile barabara za lami, inaonekana ni kama vile changarawe ngumu zilizomwagwa; je, ni kwa sababu gani Serikali haijaweka mkazo wa dhati, mahali panapoitwa Makao Makuu, kutenga pesa ya kutosha ili angalau Mji wa Dodoma uonekane tofauti na ilivyo leo na wakati wote mnatupatia maneno tu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, kwa mara nyingine, ninaomba nimjibu Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa hakika kuna mkazo mkubwa na wa dhati kabisa wa kuiendeleza Dodoma kama Makao Makuu ya Nchi yetu. Dhamira hii ipo, ndiyo maana pale fedha ilipopatikana tumeweza kutekeleza miradi michache ya kuendeleza Makao Makuu, tatizo letu ni fedha; tungekuwa na fedha tungeweza kutekeleza hata ile awamu ya tatu ya Mpango Kabambe.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa Serikali ilishaonyesha mkakati wa kuuendeleza Mji wa Dodoma kwa kujenga nyumba eneo la Kisasa, ambazo kama zingekuwepo katika sehemu nyingi, Mji wa Dodoma ungependeza; na kwa kuwa Serikali haina pesa hivi sasa; je, kwa nini hatuombi mashirika au *agents* za Serikali kama *PPF, NHC* na mashirika mengine, kuongeza nguvu na hata ikiwezekana CDA nayo badala ya kung'ang'ania nyumba ambazo zimeshakuwa za zamani, wawe wanajenga na kuuza?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, ninapenda kumjibu Mheshimiwa Dr. Zainabu Gama, Mbunge wa Kibaha, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kazi nzuri imefanywa na wakala wa majengo kujenga zile nyumba zaidi ya 300 katika eneo la Kisasa, nyumba hizi zimesaidia sana katika kupokea mradi mkubwa wa Chuo Kikuu cha Dodoma.

Kuhusu mashirika mbalimbali kujenga majengo katika Makao Makuu, ninaomba nitoe taarifa kwamba, mashirika haya kwa sasa yameshaamua kujiunga na Serikali katika kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma; mashirika hayo ni pamoja na *PPF, NSSF* na mengineyo. Wakimaliza mradi huu mkubwa wa Chuo Kikuu, bila shaka wataendelea na miradi mingine ya ujenzi.

Na. 2

**Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria**

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Kanuni ya 21(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, inabainisha kuwepo kwa Mshauri wa Bunge wa Mambo ya Sheria pamoja na majukumu yake; na kwa kuwa mambo yaliyotajwa kuyashughulikia ni mengi na ni muhimu sana:-

(a) Je, Mshauri Mkuu huyo ana watendaji wangapi wanaomsaidia katika shughuli zake za kila siku?

(b) Je, ni utaratibu upi ulioandaliwa kuwawezesha Wabunge kuitumia Ofisi hiyo ili kuweza kunufaika na huduma zitolewazo na Mshauri huyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Wete, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya mambo mapya kwenye Kanuni za Bunge letu, zilizopitishwa na Bunge hili hivi karibuni ni Bunge kuanzisha Ofisi ya Mshauri Mkuu wa Bunge kwa mambo ya sheria na majukumu yake kutajwa kwenye Kanuni hizo za Bunge.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa namna Waheshimiwa Wabunge watakavyoitumia Ofisi hiyo, pamoja na watendaji watakaokuwa wanasaidiana naye katika uendeshaji wa shughuli za kila siku unaandaliwa na ukikamilika Waheshimiwa Wabunge mtafahamishwa.

Ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, jambo hilo ni kipaumbele katika masuala muhimu yanayotekelezwa hivyo, unaombwa uvute subira.

Na. 3

**Madhara ya Utandawazi**

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza:-

Kwa kuwa, utandawazi ni mfumo wa uchumi ambao Tanzania haiwezi kuuepuka:-

Je, Serikali imejitayarisha vipi kukabiliana na madhara ya utandawazi yanayozikabili nchi zinazoendelea?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa utandawazi wa uchumi duniani ambao hauepukiki, unaweza kuwa na madhara na athari kubwa, huonekana zaidi kwenye nchi zinazoendelea. Baadhi ya athari hizo ni pamoja na rasilimali nyingi kama madini, mafuta na mazao ya misitu, kuhamishwa kutoka nchi zinazoendelea kwa malipo kidogo, hasa kwa kutumia dhana ya uwekezaji; kutokuwepo kwa usawa katika biashara, ambapo nchi maskini hazina uwezo wa kupanga bei za bidhaa zinazouza au kununua katika soko la dunia; bei hafifu kwa mazao ya kilimo; ushuru kubwa mara bidhaa hizo zinapouzwa zikiwa zimeongezwa thamani; masharti magumu katika kupatiwa teknolojia, mikopo na misaada; na hivyo kuzifanya nchi zinazoendelea kuwa na bajeti tegemezi.

Mheshimiwa Spika, ili Tanzania iweze kutumia vizuri fursa zinazojitokeza na kupunguza athari za utandawazi, Serikali inatekeleza mikakati mingi chini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na:-

- Kuongeza kasi ya upatikanaji wa elimu kwa wananchi wetu;
- Kutekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA);
- Kuimarisha miundombinu; mawasiliano, uchukuzi, barabara na nishati, ili kuongeza ufanisi katika uzalishaji;
- Kukuza biashara ya ndani na nje na kuwavutia wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi;
- Kuimarisha sekta binafsi ili iweze kushiriki kikamilifu katika uwekezaji, uzalishaji na biashara na hivyo kuinua uchumi wetu;
- Kuimarisha Kituo cha Uwekezaji ili kuweza kufanya uhamasishaji ndani na nje ya nchi;
- Kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Kikanda kama vile Jumuiya ya Afrika Mashiriki; na

- Kuimarisha ushiriki wetu na uwezo wa kujadiliana na Jumuiya za Uchumi za Kimataifa kama vile Shirika la Biashara Duniani *(WTO),* Benki ya Dunia *(WB)* na Shirika la Fedha Duniani *(IMF)* na kufikia maamuzi yenye maslahi kwa Taifa letu.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaomba nimshukuru Naibu Waziri, amenipa majibu mazuri sana, lakini ninaomba nimuulize maswali mawili madogo sana ya nyongeza. Baada ya kukiri kwake kwamba, tunapata madhara hasa sisi nchi zinazoendelea; je, Serikali imejiwekea maadili yapi ya Kitaifa kwa Lugha ya Kiingereza ya kuhakikisha kwamba, inazilinda rasilimali za nchi hii bila hata ya kujali mataifa mengine yanasema nini kama vile wafanyavyo wenzetu Waarabu?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili ni kwamba, kwa kuwa utandawazi ndiyo umefungua milango ya uwekezaji na uwekezaji huo huo ndio ukawa milango mikubwa sana ya mikataba; na kwa kuwa tumekuwa na tatizo kubwa la kuingia mikataba mibovu katika rasilimali zetu; je, Serikali kwa sasa hivi imejitayarisha vipi kupigana na kupambana na mikataba mibovu kuanzia sasa kwamba, isiwepo tena mikataba mibovu ili tuweze kulinda rasilimali zetu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza kuhusu Serikali imejiwekea *ethics code* gani ni kwamba, katika kila sekta ya uchumi wetu zinaendeshwa chini ya Sera na Mikakati Maalum, ambayo tunategemea kwamba itaheshimu uadilifu na uaminifu katika utekelezaji wake. Kwa hiyo, siyo lengo la Serikali na siyo mategemeo ya Serikali kwamba, mfanyakazi yeyote ama afisa yeyote wa Serikali, atakiuka miiko ile. Kwa nyongeza, tayari tunacho chombo ambacho kila Kiongozi wa Serikali anatakiwa aorodheshe mali zake anapoingia kwenye uongozi lakini vile vile anapomaliza uongozi. Kwa hiyo, tunategemea kwamba, zile taarifa zitakuwa za kweli na kwamba wakati inapobidi kwenda kuzikagua, zitaonekana kweli zimeonyesha uadilifu na uaminifu kwanza, kuzitoa zile lakini vile vile kwa yule afisa kufanya kazi za Serikali.

Suala kwamba Serikali ilifungua milango yake kwa utandawazi na kwa hiyo, hiyo ndiyo imepelekea tukawa na mikataba mibovu; kwanza, niseme kwamba, utandawazi siyo suala la kufungulia milango na hili siyo jambo jipya. Utawandazi ni mahusiano ya kiuchumi, ambayo hayaheshimu mipaka ya nchi na nchi, hayaheshimu mipaka ya Taifa na Taifa na hayaheshimu mipaka ya kampuni moja kwenye nchi moja kufanya biashara na nchi nyingine ama na kampuni nyingine kwenye nchi nyingine.

Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo ni lazima tukubali kuishi nalo. Kuhusu mikaba mibovu kama nilivyosema, tunatarajia kwamba, sisi viongozi tutakuwa waadilifu, tutakuwa waaminifu na kwamba kama tukifikia hapo, basi suala la mikataba mibovu litakuwa kwa kweli ni historia na hivyo ndivyo ambavyo tunaamini tutasonga mbele.

**SPIKA:** Ahsante sana. Bado tuko Wizara hiyo hiyo kwa swali linalofuata, linaulizwa na Mheshimiwa Devota Likokola, Mbunge wa Viti Maalum, Ruvuma. Kwa niaba yake, ninamwona Mheshimiwa Vita R. Kawawa. *(Makofi)*

Na. 4

**Mikopo ya Wajasiriamali**

**MHE. VITA R. KAWAWA (K.N.Y. MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA)** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi na wafugaji vijijini wanakosa fursa muhimu ya kupata mikopo ili kuwa na mitaji ya kuzalisha mali; na kwa kuwa, Serikali inaendelea kutoa vibali kwa mabenki mbalimbali kufanya biashara zao nchini:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali isiweke sharti kwa mabenki hayo kutenga hata asilimia kiasi cha bidhaa zao kukopesha wakulima vijijini?

(b) Kwa kuwa mabenki mengi yanadai mifumo ya kukopesha wananchi haijakaa vizuri hasa vijijini; je, Umoja wa Benki *(TBA),* upo tayari kushirikiana na Serikali ili kuunda mifumo hiyo mizuri hadi vijijini?

(c) Je, Serikali na mabenki hayo wapo tayari kutoa elimu ya fedha ili wananchi wasihangaike kupata mitaji na huduma nyingine za fedha?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Devota Likokola, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kufuatana na mageuzi ya sekta ya fedha nchini, yaliyoanza kutekelezwa kuanzia mwaka 1991, Serikali imejitoa katika kuhusika moja kwa moja na uendeshaji wa shughuli za mabenki na pia Serikali imeyaachia mabenki yajiendeshe kwa mfumo wa soko huria kwenye sekta binafsi. Uamuzi wa mabenki kukopesha sekta mbalimbali za uchumi wa nchi yetu ni suala la kiutendaji lililo ndani ya taratibu za mabenki hayo. Mara nyingi uamuzi huo hutokana na tathmini inayofanywa na mabenki, yakizingatia sera na masharti ya mikopo yaliyowekwa. Hivyo basi, si busara kwa Serikali kuwawekea masharti wenye mabenki na kuwashinikiza kutoa mikopo.

Hata hivyo, Serikali inatambua umuhimu wa upatikanaji wa mikopo kwa wakulima vijijini. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imekuwa ikishirikiana na kuyahimiza mabenki ya biashara nchini, kutoa mikopo kwa wakulima mmoja mmoja na pia kwa kupitia vyama vyao vya ushirika vya akiba na mikopo.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika kipengele (a) kuwa Serikali inatambua umuhimu wa kuweka mifumo bora ya ukopeshaji hadi vijijini, Serikali iko tayari kushirikiana na taasisi au chombo chochote cha kifedha kinachotambulika kisheria katika kutoa mchango wa namna gani huduma hizi za ukopeshaji zitawafikia wananchi vijijini.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali ikishirikiana na mabenki ya biashara, pamoja na Benki Kuu ya Tanzania, ipo tayari kutoa elimu ya kifedha yenye lengo la kuwaelimisha wananchi, juu ya upatikanaji wa mitaji na huduma nyingine mbalimbali za kifedha. Ningependa kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, kila mara inapohitajika, Serikali imekuwa ikishirikiana na Benki Kuu, pamoja na taasisi nyingine za kifedha, kutoa elimu ya fedha kwa wadau mbalimbali; kwa mfano, Serikali ilipoanzisha utaratibu wa ukopeshaji kwa wananchi, chini ya mpango wa uwezeshaji na kukuza ajira. Serikali ikishirikiana na Benki Kuu, *CRDB* na *NMB,* ilitoa na inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu utoaji na upatikanaji wa mikopo nchini, chini ya mpango huu.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa moja ya hatua muhimu ya kuwafikia wananchi vijijini kwa huduma za kibenki ni kuwa na benki katika Makao Makuu ya Wilaya; kwa kuwa Wilaya ya Namtumbo haina Benki ya *NMB* na *NMB* walionyesha nia; je, Serikali inaweza kutumia busara yake kutusaidia Wananchi wa Namtumbo kutuhimizia benki hiyo au benki nyingine, waweze kuja kufungua benki katika Wilaya ya Namtumbo na wawafikie wananchi kwa karibu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kwamba, wananchi ikiwezekana wote wapate huduma hizi za kibenki na kifedha na tunashirikiana kwa karibu sana na mabenki ya biashara na vyombo vingine vya kifedha, kupeleka huduma karibu na wananchi wetu.

Pamoja na Namtumbo, ninapenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, tutaendelea kama Serikali, kushirikiana na mabenki haya ya biashara pamoja na vyombo vingine vya fedha, huku tukiwahimiza kuwasogezea karibu huduma hizi za kifedha wananchi wetu, sio ngazi ya Wilaya tu lakini ikiwezekana vile vile kwenye Tarafa ili waweze kuzitumia kwa ajili ya mahitaji yao ya mitaji.

Ninapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Vita Kawawa, kwa kiasi na kadri anavyotetea jimbo lake la Namtumbo, ikiwa siyo tu kwenye fedha lakini hata kwenye zao lao la tumbaku. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, ninakushuru kwa kunipa nafasi. Haya mabenki yanafanya biashara kwa pesa za Watanzania si pesa za watu wa nje; kwa nini Serikali haiweki masharti maalumu kwa *deposit* zote za mabenki haya ambayo yanachuma pesa za Watanzania kuweka asilimia tano kila mwaka za kuwakopesha Watanzania katika nchi hii kwa kuiga mifano ya nchi nyingine ambazo zimefanikiwa sana kama vile nchi za upande wa Asia?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba haya mabenki yanafanya biashara kweli kwa pesa yetu ya Tanzania kwenye soko huria na kwenye sekta binafsi na Serikali kwa kiasi kikubwa, imesharidhia kwamba watafanya hivyo na sisi Serikali kidogo kidogo tunajiondoa. Wazo lake la kuhimiza mabenki haya kutenga kiasi fulani kwa ajili ya mikopo kwa wananchi ni wazo ambalo limesikika mara nyingi na ni kweli ninakubaliana naye, kuna nchi ambazo tayari Serikali zimeshashirikiana na mabenki yao na wakakubaliana kwamba hilo litafanyika.

Ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba na sisi siyo kwamba tumefunga masikio ama hatusikii, tutashirikiana na chama cha hawa wenzetu cha *Tanzania Bankers Association*, tuone kama hilo litawezekana. Tukikubaliana, basi watafanya hivyo.

Niseme pamoja na kutokuwepo na *percent* maalumu kwa ajili ya mikopo, ninafikiri tukubaliane kwamba, mabenki yetu haya ya biashara kwa ushirikiano wao mzuri na Serikali, yanafanya kazi nzuri sana ya kuwapa wananchi wetu mikopo.

Na. 5

**Kuboresha Mawasiliano ya Simu za Mkononi Kishapu**

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA (K.N.Y. MHE. FRED T. MPENDAZOE)** aliuliza:-

Kwa kuwa mawasiliano ya simu ni moja ya nyenzo muhimu katika kuleta maendeleo na kwa kuwa baadhi ya vijiji na Kata katika Tarafa za Mondo, Negezi na Kishapu katika Wilaya ya Kishapu havina huduma bora ya simu za mikononi; je, Serikali iko tayari kuyashawishi makampuni ya simu za mikononi kuongeza minara ya simu katika maeneo hayo ili kuboresha mawasiliano?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Fred Mpendazoe, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Simu ya *Vodacom* imekwishaanza mchakato wa kiufundi kwa ajili ya kuleta mawasiliano katika maeneo ya Kishapu. Kwa sasa tayari

Kampuni hiyo imeweka mtambo wake katika Makao Makuu ya Wilaya ya Kishapu. Mara tu mchakato huu wa kifundi utakapomalizika, maeneo yote ya Wilaya ya Kishapu, ikiwa ni pamoja na maeneo ya Vijiji na Kata katika Tarafa za Mondo, Negezi na Kishapu, yatanufaika na huduma hii.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Celtel* imeshajenga mnara katika eneo la Kishapu na kufikisha mawasiliano katika eneo hilo na maeneo ya jirani. Aidha, Kampuni ya *Celtel,* inaendelea kufanya tafiti katika maeneo ya Mondo na Negezi ili kufikisha mawasiliano ifikapo Mei, 2008.

Mheshimiwa Spika, katika mradi wake wa kusambaza mawasiliano nchi nzima, Kampuni ya *Zantel* iko katika hatua ya kujenga minara ya mawasiliano katika maeneo ya Kishapu, Mipa na Mhunze, ambayo itaweza kutoa mawasiliano katika Tarafa za Mondo na Negezi. Minara hii itaanza kuhudumia wateja ifikapo Septemba, 2008.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Kampuni ya Simu ya *Tigo,* inayafanyia upembezi yakinifu maeneo ya Tarafa za Mondo, Negezi na Kishapu ili kuyaingiza katika mipango yake ijayo.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Simu ya *TTCL* ipo katika mikakati ya kusambaza na kuboresha huduma ya simu za mikononi, kwa kutumia teknolojia iitwayo *Code Division Multiple Access (CDMA)* katika maeneo mbalimbali nchini. Huduma hii ya mawasiliano iliyoanzishwa mwaka 2007, tayari inapatikana katika Miji Mikuu ya Mikoa na baadhi ya Miji ya Wilaya. Katika Mkoa wa Shinyanga, simu za mkononi za *TTCL,* tayari zinapatikana maeneo ya Shinyanga Mjini, Kahama, Mwadui, Maswa, Bariadi, Meatu na Tinde. Utekelezaji wa mradi huu, unafanyika kwa awamu na Wilaya ya Kishapu ni miongoni mwa maeneo ambayo *TTCL* imelenga kupeleka huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, gharama za ujenzi wa minara na uwekaji wa mtandao wa mawasiliano ni kubwa na hugharimu fedha nyingi ukilinganisha na mwelekeo wa kibiashara wa baadhi ya maeneo. *TTCL* itaendelea kujumuisha maeneo hayo katika mradi wa upanuzi wa mtandao, kadri fedha itakavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, itaendelea na jitihada zake za kuyashawishi makampuni ya simu za mikononi, kuongeza na kuboresha huduma za mawasiliano nchini, hasa maeneo ya vijijini ambako mahitaji ya maendeleo ni muhimu sana.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri na ninaomba tu nisisitize majibu yake alivyosema, ndani ya mwaka huu, baadhi ya maeneo yatakuwa yamepata mawasiliano na ninaamini wananchi wa Wilaya ya Kishapu watafurahi sana. Baada ya shukrani hizo, ninaomba niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa matatizo ya mawasiliano yaliyoko Kishapu yanafanana na kukaribiana na tatizo lililoko Bukombe; na kwa kuwa katika Wilaya ya Bukombe iko minara maeneo ya Masumbwe lakini inakamata umbali mfupi sana kiasi kwamba, maeneo ya Rugunga ambako kuna wafanyabiashara wengi sana hawapati mawasiliano haya; na kwa kuwa nilikwishaandika barua kwa Mheshimiwa Waziri; je, anaweza akatusaidia makampuni haya yaongeze nguvu kwenye maeneo hayo ili wananchi wa maeneo yale wapate mawasiliano au anaweza akashauri makampuni haya yakaweke mnara maeneo ya Nyasato ambapo itakamata eneo kubwa la Wilaya ya Bukombe? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ninakubaliana naye kwamba, alileta malalamiko yake ya masuala ya simu katika maeneo yake na tumeyafanyia kazi ni bahati mbaya tu hawajafika wenzangu wanaohusika na mawasiliano kule. Ninapenda nimhakikishie kwamba, nitawasiliana nayo tena makampuni ya simu, kuona kama uko uwezekano wa kuweka mnara hapo anapopazungumzia yeye (Nyasato), baada ya makampuni hayo kufanya utafiti ipasavyo. Ninapenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, nia ya Serikali ni kuona vijiji vyote vinapata mawasiliano ya simu ili wananchi waweze kufanya shughuli zao za maendeleo kwa urahisi zaidi.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kuniona. Pamoja na huduma nzuri zinatolewa na makampuni mbalimbali ya simu za mikononi, bado kuna tatizo la simu hizo kutokufika maeneo ya mabondeni; na kwa kuwa mtu anaweza akapata tatizo hata eneo la bondeni na akashindwa kupata msaada; je, makampuni haya yana mikakati gani ya kuona kuna tatizo gani simu za mikononi kutokushika maeneo ya mabondeni?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwenye maeneo ya mabondeni, mawasiliano yanakuwa ni dhaifu na hata kwenye maeneo ambapo ni msitu mnene mawasiliano yanakuwa ni dhaifu. Hivyo ni juu ya makampuni haya kuona ni teknolojia gani inafaa katika maeneo hayo. Hilo ndilo linalowafanya kuchukua muda kufanya utafiti, kuona ni teknolojia gani ya mawasiliano inaweza kufaa kwa maeneo kama hayo. Labda nimkumbushe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, juhudi zinafanywa.

Ninapenda niyashukuru makampuni ya simu za mikononi kwa kazi nzuri zinazofanywa; maeneo mengi tu ya Mkoa wa Singida ambapo Mheshimiwa Mbunge anatoka, yamefikiwa. Tutazidi kuwasiliana na makampuni haya, waone ni namna gani wanaweza kuwafikia wananchi walioko mabondeni, lakini ninadhani tukubaliane kwamba, maeneo mengine ya mabondeni si vizuri kukaa, kwa sababu mvua zikinyesha zinaweza zikaleta athari kwao.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri na tunashukuru kwa tahadhari hiyo. Tunahamia sasa Wizara ya Miundombinu, swali linaulizwa na Mbunge wa Tandahimba, Mheshimiwa Abdallah Juma Njwayo.

Na. 6

**Matumizi ya Bandari ya Mtwara**

**MHE. JUMA A. NJWAYO** aliuliza:-

Kwa kuwa Bandari ya Mtwara haiko kwenye mtandao unaoonyesha kuwa ni mojawapo ya Bandari za Tanzania inayoweza kutumika kushushia mizigo toka nje *(destination),* hivyo kusababisha wananchi wenye nia ya kushusha mizigo yao katika bandari hiyo kushindwa kufanya hivyo; na kwa kuwa hivi karibuni Kampuni ya Utafiti wa Mafuta - *UP STREAM,* iliweza kushusha magari 72 na makontena 40 kwa muda wa *shift* moja (kuanzia saa 9.00 alasiri hadi saa 5.00 usiku), jambo linalodhihirisha kuwepo kwa vifaa vya kutosha bandarini hapo:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ni vyema sasa bandari hiyo ikawekwa kwenye mtandao ili iweze kupunguza msongamano uliopo katika Bandari ya Dar es Salaam?

(b) Kwa kuwa Bandari ya Mtwara ni moja ya miundombinu iliyoko kwenye Mpango wa Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara *(Mtwara Corridor);* je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuanza kuitumia bandari hiyo ya Mtwara kikamilifu?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA),* ina tovuti yake, yaani www.tanzaniaports.com ambapo bandari zake zote ikiwemo Bandari ya Mtwara zimeainishwa. Mtandao huu, unatumika katika kutangaza shughuli za Mamlaka na Bandari zake na una taarifa muhimu ambazo wananchi au wafanyabiashara ndani na nje ya nchi, wenye nia ya kutumia bandari wanaweza kuzihitaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba, kwa sasa Bandari ya Mtwara haitumiki kikamilifu kwa sababu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na miundombinu duni na ukuaji hafifu wa uchumi Ukanda wa Kusini. Serikali ina mikakati mbalimbali ya utekelezaji chini ya Mpango wa *Mtwara Development Corridor* na *Tanzania Mini-Tiger Plan 2020*, yenye lengo la kukuza uchumi wa ukanda wa Mtwara na hivyo kuitumia kikamilifu bandari hiyo. Serikali kwa kutumia mamlaka ya usimamizi wa bandari, ina mpango pia wa kupanua Bandari ya Mtwara, sambamba na kukuza shehena ipitayo kwenye bandari hiyo, kwa kuanzisha eneo la *EPZ.* Chini ya mpango huu, ekari 2,646 zimenunuliwa tayari ili zitumike kwa ajili ya upanuzi wa bandari na shughuli za *EPZ.*

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imedhamiria kujenga barabara kutoka Masasi hadi Mbamba Bay kwa kiwango cha lami na hivi sasa tuko katika hatua mbalimbali za

utekelezaji. Hii ni dhahiri kwamba, kukamilika kwa barabara hiyo, kutawavutia wawekezaji katika nyanja za kilimo, viwanda, madini, misitu na uvuvi na ni wazi kwamba, mafanikio ya miradi hii, yataongeza shehena katika Bandari ya Mtwara na hivyo kupunguza msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam na pia kuinua shughuli za kiuchumi na kijamii katika ukanda huu.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Ahsante kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa yapo mazungumzo yaliyokuwa yanaendelea kati ya Kampuni ya *EMERETS SHIPPING LINE,* ambayo ipo tayari kufanya *trans-shipment* katika Bandari ya Mtwara lakini hadi sasa mazungumzo hayo yana dalili ya kukwama; je, Serikali inaweza kulieleza Bunge hili, kuna ugumu gani wa kufikia makubaliano ya haraka ili bandari hiyo ya Mtwara iweze kuneemeka?

Pili, Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa anajibu swali la Mheshimiwa Mohamed Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini, katika Mkutano wa Kumi, aliliambia Bunge hili kwamba, mwezi Februari bandari hiyo ingeweza kufanya kazi kwa ukamilifu; lakini hapa tunapoongea leo ni Aprili nini kimejiri?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, wapo watu ambao wameomba Bandari ya Mtwara ili waweze ku-*off load* makontena Mtwara na shughuli hizo ni lazima kwanza uzifanyie utafiti na tulitegemea utafiti na uchambuzi wa makampuni haya yaliyoomba, ungemalizika mwezi Februari mwaka huu lakini bado hawajamaliza. Kwa sababu lazima umjue yule anayetaka kufanya biashara ana uwezo kiasi gani. Ninategemea muda si mrefu, masuala haya yatapatiwa ufumbuzi.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari, yaani *TPA,* wamekubaliana na baadhi ya wenye meli katika jitihada za kupunguza msongamano wa bidhaa na makontena bandarini kwamba, meli kubwa ziende moja kwa moja mpaka Mtwara zipakue na kisha meli ndogo zichukue mizigo kutoka Mtwara kupeleka Dar es Salaam au kwa njia nyingine ya barabara, lakini utaratibu huu umekataliwa na *TRA.* Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuzungumza na Waziri wa Fedha ili kusaidia makubaliano haya ya *TPA* na wenye meli ya kupeleka mizigo bandarini ili kufanikisha jambo hili mapema iwezekanavyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, ingelikuwa kweli ni busara meli kubwa zingeweza kupeleka mizigo yao ku-*off load* Mtwara na meli ndogo ndogo zikaweza kuchukua mizigo ile kuirudisha Dar es Salaam. Nikubaliane naye tu kwamba, tutamwomba Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, aweze kukaa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kuona ni namna gani wanaweza kutatua suala hili kwa njia ya wepesi zaidi.

Vile vile nitoe wito kwa wale ambao wanazo meli ndogo ndogo, kwa sababu zilizoko ni chache, waweze basi kujitokeza kuwekeza katika maeneo hayo ili usafiri uwe mwepesi, isiwe makontena yakifika Mtwara yanakwama tena kurudi Dar es Salaam.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunahamia sasa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Swali linalofuata ni la wale waliotoka nje. Kwa hiyo, ninaliacha. Swali linalofuata ni la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza.

Na. 8

**Upatikanaji wa Hatimiliki**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilitoa sehemu ya ardhi ya Mashamba ya Azimio Ranchi, Kibaranga na *Mlingoti Sisal Estate,* kuwapimia eka tano kwa kila mmoja na kupewa hati ya *Offer:*-

(a) Je, Serikali itarekebisha hatimiliki za awali ili kuwezesha waliopata *Offer* kupewa hati mpya ya kumiliki kwa mgao wa sasa?

(b) Ikiwa kuna tatizo la kutolewa kwa hati mpya, je, Serikali itawasaidia vipi Idara ya Ardhi ya Wilaya ya Muheza kufanya marekebisho yanayohitajika kisheria ili kuwezesha hatimiliki za mgao wa sasa kutolewa?

(c) Je, hali iko vipi kwa sehemu za maeneo ya mashamba hayo kwenye vijiji vya Mwarimba, Mbuyuni, Mabungo, Misozwe na Kichemba?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilimega ardhi kutoka kwenye mashamba yaliyokuwa ya Mamlaka ya Mkonge na kugawa eka tano tano kwa wananchi wanaozunguka mashamba hayo. Hata hivyo, mashamba hayo hadi sasa bado yanayo hati miliki zilizo hai za iliyokuwa Mamlaka ya Mkonge. Serikali iliweka chini ya *PSRC* mali mbalimbali zilizokuwa chini ya Mamlaka ya Mkonge, ikiwa ni pamoja na mashamba haya.

Kutokana na uhakiki wa upimaji wa awali ilibainika kuwa, upimaji uliofanywa haukuzingatia makubaliano ya awali kati ya Mamlaka ya Mkonge na wananchi. Hivyo, Wizara yangu iliiagiza *PSRC,* kurejea upimaji huo kwa kuzingatia makubaliano ya awali. Kwa hivi sasa Wizara yangu inafuatilia kwenye malaka iliyopewa jukumu la kusimamia kazi za *PSRC,* ambayo ni *M/S Consolidated Holdings Company Ltd.,* ili wakamilishe upimaji huo. Pia imeitaka Kampuni hiyo irejeshe Serikalini, hatimiliki za mashamba hayo ili zifanyiwe marekebisho na hatimaye wananchi waweze kupewa hatimiliki mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, mara upimaji mpya wa mashamba hayo na hatua nyingine za umilikishaji kwa mujibu wa sheria zitakapokamilika, Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, itatoa hatimiliki kwa wananchi husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba, wananchi wa vijiji vya Mwarimba, Buyuni, Misozwe, Mabungu na Kicheba, wana uhaba wa ardhi. Wananchi wa vijiji hivi, wamekuwa wakiomba Serikali iwaongezee ardhi kutoka kwenye mashamba hayo. Vijiji hivi vilikwishamegewa hekta 3,780 kati ya 9,510 kutoka kwenye mashamba yanayozunguka vijiji husika, eneo lililobaki la hekta 5,730 limeendelea kuwa chini ya Serikali kupitia kwa mrithi wa *PSRC*. Mnamo Septemba, 2007, Wilaya ya Muheza, iliwasilisha mapendekezo ya kufuta hati miliki ya baadhi ya mashamba kwa nia ya kuviongezea ardhi vijiji vinavyozunguka mashamba hayo. Wizara yangu kwa kushirikiana na mamlaka iliyoachiwa mashamba hayo, inalifanyia kazi ombi hili la Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa. Hata hivyo, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Kimsingi matatizo makubwa katika maeneo ambayo yamekwishatolewa ni kwamba, Serikali za Vijiji pamoja na Halmashauri wamekuwa hawana fedha za kuyapima mashamba yale na kugawa vizuri kwa wananchi wanaohusika. Ninaishukuru sana Serikali ya Uingereza, kupitia Serikali ya Ireland, kupitia kwa *Irish Aid,* ambao walisaidia sana upimaji katika Shamba la Azimio. Je, Serikali inasema nini katika kuandaa utaratibu wa kuzisaidia Serikali za Vijiji na Halmashauri, kuwezesha kupima ardhi hiyo vizuri na kuigawa kwa wananchi wake hasa kwa kuwapa fedha?

Pili, huyu mrithi wa *PSRC* mara nyingi kumetokea matatizo, wanafanya kazi bila kushirikisha Halmashauri au kushirikisha hata Serikali za Vijiji. Je, Serikali itasaidia kuona kwamba, kwa hivi sasa hawa wanaofanya kazi hizi, wanaishirikisha vizuri Halmashauri ya Wilaya ya Muheza na vile vile Halmashauri ya Vijiji vinavyohusika ili kusitokee migongano isiyokuwa na sababu?

Je, serikali itasaidia kuona kwamba kwa hivi sasa hawa wanaofanya kazi hizi wanaishirikisha vizuri Halmashauri ya Wilaya ya Muheza na vilevile Halmashauri za vijiji vinavyohusika ili kusitokee migongano isiyokuwa na sababu?

**WAZIRI WA ARDHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la kwanza, kwamba Serikali za vijiji na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza hawana fedha za kupima mashamba hayo wameomba Wizara yangu isaidie. Ningependa tu kushauri kwamba Halmashauri ya Muheza, inazo fursa za kutafuta fedha sehemu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukopa kutoka kwenye mfuko wa *Local Government Loans Board,* wanaweza kukopa pesa hizo na wakapima. Vilevile pale Wizarani tunao mfuko unaozunguka na baadhi ya Halmashauri wameshaomba na tumeshawakopesha ikiwa ni pamoja na Morogoro, Mbeya, Kibaha, Mwanza na kadhalika. Kwahiyo, vilevile Halmashauri ya Muheza wanaweza kuleta maombi kukopeshwa katika mfuko huu ambao ni mfuko maalum wa kukopesha Halmashauri kwa kupima viwanja na mashamba.

Kuhusu mrithi wa *PSRC* kufanya kazi bila kushirikisha Halmashauri za Vijiji wala Halmashauri za Wilaya, kwakweli hiyo ni dosari. Siku zote Serikali yetu inahimiza kwamba Serikali inapofanya kazi na wananchi ni lazima tuwe na mipango shirikishi. Kwahiyo, kama kweli hawawashirikishi tutawajulisha ili wafuate haya maadili ya kushirikisha wananchi katika shughuli za Serikali.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ilikuwa tuwaite wanaouliza maswali haya ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, lakini wote ni Kambi ya Upinzani na hawapo. Kwahiyo, tutakwenda sasa Wizara ya Katiba na Sheria na nimearifiwa kwamba Dr. Harrison Mwakyembe, ambaye amekwenda Mbeya, Jimboni kwake ambako kuna mafuriko makubwa sana, amemuachia Mheshimiwa Ruth Msafiri aulize swali kwa niaba yake.

Na. 11

**Kufutwa kwa Sheria Zinazobagua Wanawake**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI (K. N. Y. MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE)** aliuliza**:-**

Kwa kuwa, katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalinda usawa wa binadamu na stahili ya mtu kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake na inapiga marufuku sheria yoyote yenye ubaguzi wa dhahiri; na kwa kuwa mwaka 1994 Mahakama Kuu ya Tanzania kwa kuzingatia msingi huo wa Katiba ilipiga marufuku kifungu cha sheria ya mila ya Kihaya *(Haya Customary Law (Declaration) Order of 1963)* ambacho kinambagua mwanamke asirithi ardhi na kuuza alichokirithi tofauti na mwanaume:-

(a) Je, ni nini kinachozifanya Mahakama zetu kuendelea kuzikumbatia sheria za mila zilizokwishapigwa marufuku kwa kumbagua mwanamke?

(b) Je, ni kitu gani kinachoipa Serikali kigugumizi kuifutilia mbali sheria hiyo ya Kihaya ili isiendelee kuwachanganya wenye kusimamia utoaji haki?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Dr. Harrison Mwakyembe, Mbunge wa Kyela, lenye sehemu (a) na (b), napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu, Mahakama ndicho chombo pekee chenye dhamana ya kutoa haki. Mahakama hufanya hivyo kwa kutoa

tafsiri sahihi ya sheria za nchi kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na mazingira halisi ya kesi husika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwakyembe, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mahakama za chini ya Mahakama Kuu zinapaswa kuheshimu, kuzingatia na kufuata uamuzi unaotolewa na Mahakama Kuu pale zinapofanya maamuzi katika kesi mbalimbali. Hivyo basi, iwapo kuna Mahakama ya chini ya Mahakama Kuu ambayo bado inaendelea kutoa uamuzi kwa kufuata sheria ya kimila iliyobatilishwa na Mahakama Kuu, Mahakama hiyo inafanya hivyo kwa makosa.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa wito kwa Mahakama zote nchini kuheshimu, kuzingatia na kufuata maamuzi ya Mahakama Kuu au ile ya Rufani.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taratibu za kisheria, sheria yoyote inayobatilishwa na Mahakama hususan Mahakama Kuu au ile ya Rufani, basi sheria hiyo huhesabika kuwa imefutwa. Hivyo basi, sheria ya kimila aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge, imehesabika kuwa imefutwa katika vitabu vya sheria vya nchi hii.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri tena kimsingi ningetakiwa kusema yanaridhisha kuhusu kufutwa kwa kifungu hiki cha 20 cha Sheria ya Mila ya Kihaya ambacho kimsingi kinambagua mwanamke asirithi ardhi na kuuza alichokirithi tofauti na mwanaume:-

Je, Serikali ina taarifa kwamba katika Mkoa wa Kagera wanawake wajane na watoto wa kike wanaozaliwa katika familia au katika koo wanaendelea kunyanyaswa na kubaguliwa kuhusu kurithi ardhi katika ardhi za familia au ardhi ya ukoo kwa kutumia kifungu hiki?

Pili, kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba kifungu chochote ambacho kimefutwa na Mahakama Kuu hakiruhusiwi kutumika tena na Mahakama za ngazi zinazifuata, yaani kinahesabiwa kimefutika, atakuwa tayari kuutembelea Mkoa wa Kagera, akakutana na wanawake wajane na hao akina dada ambao wananyanyaswa na sheria hii ili kuweza kuwasikiliza na kuwasaidia kuzifuta kesi zote zilizo katika Baraza la Ardhi na Wilaya ambalo linatumika hasa kwa eneo la Bukoba Mjini ili kuweza kuwasaidia kuondokana na tatizo hili na kuwapa haki za kurithi ardhi za waume zao na kurithi ardhi katika koo zao na kupata haki za kuziuza tena pale wanapotakiwa kuziuza?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nataka nikiri kwamba kwa kweli sina taarifa kwamba wanawake wajane na wanawake ambao wanastahili kurithi mali za nduguzao kwa upande wa kiume wanafanyiwa vibaya, wanadhulumiwa kule Kagera. Kama ni hivyo inatokea kweli, naomba kwanza nitoe wito kwa uongozi wa Kagera uliopo kuhakikisha kwamba hali kama hiyo inakwisha mara moja.

Lakini pili, nikijibu swali lake la pili, nataka nimuahidi kwamba nitachukua muda nije na wataalamu tukae tuwaone hawa wanawake wanaoteseka, wanaonyanyaswa na kudhulumiwa ili tuone ni kitu gani tunaweza kufanya kuwaondoa katika hali hiyo. Nataka niseme tu kwamba Serikali haisimamii unyanyasaji au uonevu wa wanawake mahali popote pale katika shughuli yoyote ile iwe ya mirathi au shughuli nyingine yoyote.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaendelea, nalazimika nikumbushe kuhusu Kanuni ya 66, fasili ndogo ya 3(b). Inasema hivi, *"Mbunge aliyepo Bungeni wakati wote wa mjadala atatakiwa kutulia na kukaa kwa heshima mahali pake na hatatangatanga kwenye ukumbi wa Mikutano bila sababu."* Kuna Mheshimiwa mmoja leo nimemwangalia amefanya kosa hili, amekwenda kila mahali sijui ana kitu gani? Namwomba atulie. Kama ana haja ya mawasiliano, basi atafute njia nyingine kuliko kutangatanga ndani ya Ukumbi.

Tunaendelea, wengine wanaita ubabe wa Spika huo, lakini ndio Kanuni zinavyosema. Swali linalofuata ni la Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, linaulizwa na Mheshimiwa Saidi Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge. *(Kicheko)*

Na. 12

**Mafunzo ya J.K.T.**

**MHE. SAID J. NKUMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa JKT ilitumika kuwaandaa vijana, kuwa na uvumilivu; na kwa kuwa vijana wengi wanaopata ajira wanashindwa kuishi vijijini kwa kushindwa kumudu maisha katika mazingira hayo:-

Je, Serikali itaandaa utaratibu wa kurudisha mafunzo hayo kwa wahitimu wanaomaliza vyuo tayari kwa ajira za kada mbalimbali?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Nkumba, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Kwanza, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa JKT ilifanikiwa kuwajenga vijana kuwa na moyo wa uvumilivu na kuweza kuishi katika mazingira mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa Na.16, sura ya 533 ya mwaka 1964 iliwahusu vijana wenye elimu ya msingi na siyo wenye elimu ya juu. Kwa kuzingatia kasoro hiyo, mwaka 1966 Serikali kupitia Bunge lake ilifanya marekebisho ya sheria hiyo kwa kuwachukua vijana wote wenye elimu ya kidato cha sita na vyuo

kujiunga na JKT kwa mujibu wa Sheria. Hata hivyo, mwaka 1994 Serikali ilisitisha utaratibu huo kutokana na kupungua uwezo wa kuendesha shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2001, Serikali ilirejesha tena shughuli za JKT kwa vijana wa kujitolea (*volunteers*). Aidha, kufikia mwaka 2010, Serikali imedhamiria kuanzisha pia utaratibu wa kuwachukua vijana waliomaliza kidato cha sita na vyuo kwa mujibu wa Sheria baada ya kubaini athari za kimaadili zinazojitokeza miongoni mwa vijana kuiga tamaduni za kigeni kwa kuzingatia mabadiliko ya mfumo wa maisha duniani hasa utandawazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaanza maandalizi hayo kwa kukarabati majengo na miundombinu mingine kama vile mifumo ya umeme na maji. Aidha, juhudi zinafanyika pia kuandaa walimu wa kutosha kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaandaa mpango mzuri kutekeleza wajibu huo kwa kuzingatia uwezo wa Serikali na wingi wa vijana uliopo.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika,nashukuru sana. Baada ya majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa vijana wanaojiunga na JKT kwa mfumo wa sasa wanapata mafunzo na baada ya hapo wanarudi nyumbani, wanaishi bila ajira zozote, Serikali kwanini isione umuhimu wa kuunda vikosi vya kazi vijijini kwa kutumia vijana hawa wanaomaliza mafunzo haya ili waweze kuleta maendeleo vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Said Nkumba. Tumeipokea changamoto yake ya umuhimu wa kuona uwezekano wa kuunda vikosi kazi katika vijiji mbalimbali kwa kutumia vijana tuliowafundisha katika JKT. Lakini mkazo mkubwa wa JKT ni kufanya vijana wapate mwamko wa kujitegemea, kufikiri na kubuni kazi za kufanya huko waliko.

Kwa hiyo, pamoja na changamoto hiyo na utaratibu tulionao, tutaendelea nao pamoja na kutafakari kwa makini zaidi namna ya kufanikiwa.

Na.13

**Orodha ya Askari Waliopata Ulemavu Wakati wa Vita vya Nduli Iddi Amin**

**MHE. HAROUB SAID MASOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakati wa vita vya Nduli Idd Amin kulikuwa na wanajeshi wengi wa Tanzania waliofariki na wengine kupata ulemavu wa maisha na kwa kuwa waliopatwa na majanga hayo walikuwa kazini wakitetea nchi yao:-

(a) Je, Serikali inayo orodha ya wapiganaji waliopata ulemavu ambao wako hai hadi sasa hapa nchini?

(b) Kama orodha na anuani zao zipo, Serikali inawasaidia vipi hasa kupatiwa vifaa kama baiskeli maalum na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Masoud, Mbunge wa Koani, lenye sehemu (a) na (b) kama lifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kupitia Jeshi la Wananchi wa Tanzania, *JWTZ*, inayo orodha ya walemavu wa vita 121 ambao wako hai na wamegawanyika kama ifuatavyo:-

Walioko kwenye utumishi wa Jeshi mpaka sasa ni 63, walioko kwenye utumishi wa umma ni sita na waliostaafu baada ya kufikia umri au ugonjwa ni 52.

(b) Mheshimiwa Spika, walemavu wa vita ya Kagera huwasilisha maombi yao ya mahitaji ya vifaa mbalimbali Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na kwa kutegemea bajeti yetu, baadhi yao hupatiwa misaada kulingana na uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Spika, wako walemavu ambao wamepatiwa baiskeli, pikipiki pamoja na *tool box* na wengine viungo bandia.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia Makao Makuu ya Jeshi, walemavu 12 wanaendelea kubadilishiwa viungo mbalimbali vya bandia kwa kuzingatia ulemavu walionao.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, swali hili nimeliuliza baada ya kupata manung’uniko kutoka baadhi ya wanajeshi ambao hawapatiwi msaada kama ilivyoelezwa hapa, na kwa kuwa wanajeshi hao waliostaafu ni miongoni mwa hao 52; Je, Mheshimiwa Waziri, atakubali kulitangazia Taifa kwamba miongoni mwa hao 52 wajiorodheshe kwenye Kambi za Majeshi ili waweze kupata misaada hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Haroub, kama ifuatavyo:-

Kwanza niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba orodha tunayo. Ninachoweza kumuhakikishia Mheshimiwa Haroub ni kwamba, tutaifanyia kazi orodha hii kwa kasi zaidi ili isiwepo sababu yoyote ya kuandika orodha upya.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wapiganaji wetu ni watu muhimu sana na Serikali haina budi kuwalinda na kuwaenzi kama wao wanavyolinda nchi yetu na kwa kuwa baadhi ya wapiganaji wetu hupoteza viungo na maisha yao pale wanapokwenda vitani; Je, Serikali ina mkakati gani muhimu, maalum wa kuwawekea bima ya maafa na maisha wapiganaji wetu wanaokwenda vitani?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba, utaratibu tulionao mpaka sasa hivi wa kusaidia askari wetu wanaopata maafa katika vita na shughuli zao za kikazi bado sio mbaya. Lakini wazo la kuwa na bima kwa ajili ya askari wetu ni wazo jema, tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika Bunge hili Tukufu Serikali ilitoa kauli kwamba wale askari wote waliopigana katika vita vya Idd Amin Dada, watapatiwa fedha kwa kila mwezi. Je, hatua hii imefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, utaratibu wa Serikali wa kuwalipa askari wake waliopigana vita wakati wa Idd Amini haujabadilika, uko vilevile tunaendelea kuwalipa hatua kwa hatua.

Kinachoongelewa ni kasi ya kuhakikisha kwamba tunawalipa wote vizuri lakini kwa muda wanaomaliza kazi zao. Kwa mfano, wale ambao wapo kazini sasa hivi hawalipwi mafao yao ya uzeeni mpaka watakapokuwa wamestaafu.

Kwa hiyo, hatuwapuuzi, tunawapa uzito unaostahili na tunatambua kazi kubwa waliyoifanya kwa niaba ya Taifa letu.

Na.14

**Kuajiri Askari Wanyamapori katika Mbuga ya Wanyama ya Selous**

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA** aliuliza:-

Kwa kuwa Jimbo la Kilwa Kaskazini limepakana na Mbuga ya Wanyamapori ya *Selous* na kwamba kuna uharibifu mkubwa wa mazao kutokana na wanyamapori kama vile ndovu: Je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri askari wanyamapori wa kutosha ili kunusuru mazao na kudhibiti tatizo la njaa linalotokea mara kwa mara?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, awali kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Samsoni Mpanda, naomba kwa ruksa yako nitoe shukrani zangu kwa Mheshimiwa Rais, kwa kuniona, kuniamini na kunipa majukumu haya ya ziada. Lakini pia niwashukuru sana

wananchi wenzangu wa Jimbo la Msalala ambao daima tumekuwa pamoja na hata kwenye hili wameniahidi kwamba tutakuwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya salamu hizo za shukrani, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Samsoni Mpanda, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kama yalivyo maeneo mengine yanayopakana na hifadhi za wanyamapori, Jimbo la Kilwa Kaskazini linalopakana na pori la akiba la *Selous.* Jimbo la Kilwa limekuwa likiathirika kutokana na uharibifu wa mazao ya wananchi mara kwa mara unaosababishwa na wanyamapori waharibifu hususani tembo, viboko na nyati. Tatizo hili linakuwa kubwa katika Jimbo la Kilwa Kaskazini, kwasababu ya wanyama kuwa wengi na maeneo ni makubwa kwa kulinganisha na idadi ya askari wanyamapori wasiozidi wanne walioajiriwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa. Hivyo, Wizara yangu inakabiliana na tatizo la wanyamapori wakali na uharibifu kama ifuatavyo:-

Kwanza kutumia watumishi wa Idara ya Wanyamapori hususani pori la akiba la *Selous* pamoja na kikosi dhidi ya ujangili *KDU* Songea ambao hushirikiana na askari wanyamapori wachache walioko kwenye Halmashauri ya Kilwa kudhibiti wanyamapori waharibifu pindi wanapopokea taarifa kutoka vijiji vilivyo jirani na pori la akiba la *Selous*.

Mheshimiwa Spika, ajira Serikalini hususan Idara ya Wanyamapori inakwamishwa na ukosefu wa waombaji wenye sifa kwenye soko la ajira. Mfano katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 Serikali imetangaza nafasi 80 za ajira ya Mhifadhi wa Wanyamapori Daraja la Pili. Ni waombaji 43 tu ndio waliojitokeza kuomba nafasi hizo. Hata hivyo, kwa kutambua kuwa maeneo yenye wanyamapori ni makubwa kwa kuyalinda, wakati ambao idadi ya askari wanyamapori ni ndogo, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Ubelgiji imeanzisha Mradi wa Ushirikishaji wa Jamii katika Uhifadhi yaani, *Eastern Selous Community Wildlife and Natural Resources Management Project,* ambao unalenga katika kushirikisha wananchi katika uhifadhi wa wanyamapori na mazingira *(Maliasili)* ya Wilaya ya za Kilwa na Rufiji.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu unashirikisha jumla ya vijiji tisa vya Wilaya ya Kilwa na vijiji 13 vya Wilaya ya Rufiji. Hadi sasa mradi huu umekwishatoa mafunzo kwa askari 45 katika Kituo cha Mafunzo cha Wanyamapori, Jamii Likuyu Sekamaganga Wilaya ya Namtumbo. Mafunzo haya yanalenga katika kuwajengea uwezo kwa kusimamia rasilimali za wanyamapori katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na kulinda mali na maisha ya wananchi dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kushirikisha wananchi ,Wizara itaendelea kutekeleza jukumu la kuwalinda wananchi na mali zao dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu katika Jimbo la Kilwa Kaskazini kama iklivyo kwingineko nchini ili kunusuru mazao na kudhibiti tatizo la njaa linalotokea mara kwa mara. Aidha, Wizara itaendelea kuishauri Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kuajiri askari wanyamapori ili kukidhi

mahitaji ya Wilaya ya Kilwa. Wakati huo Wizara nayo itaendelea kuomba kibali cha kuajiri kila mwaka kuongeza idadi ya askari kwenye vituo vya *Selous* Kanda ya Miguruwe na Kikosi dhidi ya Ujangili Kanda ya Kusini Songea.

**MHE. SAMSON F. MPANDA:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu mazuri yalioyotolewa na Naibu waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, ifikapo wakati wa njaa nitakapokuja kuomba chakula kwasababu ya uharibifu uliotokea na wanyama waharibifu: Je, nitapata kipaumbele kama inavyotakiwa?

Pili, je, Wizara inao ufahamu kwamba kuna wanyama kama nguruwe au viboko maji bahari ambao vilevile wanadhuru wananchi wa Kinjumbi, Mingumbi, Kipatimu na sehemu nyingine zote ambazo zinaweza kudhuriwa na hawa wanyama? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu msaada wa chakula endapo njaa itatokea, kama tulivyosema kwenye jibu letu la msingi kwamba katika maeneo ambayo kuna uharibifu wa mazao unaotokana na wanyamapori hasa kwenye Jimbo la Kilwa Kaskazini, Serikali imeandaa huu mpango wa kushirikisha wananchi ili kuhifadhi mazingira hususani ya wanyamapori na katika kufanya hivyo wananchi wanapata mafunzo ya kujihami na wanyama hao.

Lakini pia wanapewa taaluma ya kuweza kutambua viashiria vya awali vya kwamba yawezekana muda fulani kunaweza kukatokea tatizo la wanyamapori na hivyo kuiarifu Wizara mapema kabla tatizo halijatokea.

Kwa hivi sasa *cases* zinapojitokeza kwamba tatizo tayari limeshajitokeza Wizara imekuwa ikishirikiana na wananchi wa maeneo husika kwa kuwasaidia pale ambapo inawezekana. Kwa sasa hivi utaratibu wetu ni kwamba pale ambapo wanyama wanakuwa wameharibu maeneo ya hasa ma zao sisi huwa tunatoa kifuta jasho cha shilingi laki moja kwa shamba ambalo linazidi heka moja ambalo linakuwa limeharibiwa kabisa.

Kwa maana hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge, tutumie vizuri huu mradi ambao tayari upo kwenye Jimbo lake, lakini pia tuwasiliane kila linapotokea tatizo ili kuweza kukabili tatizo badala ya kusubiri msaada pale ambapo tatizo linakuwa limeshatokea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wananchi wengine wanaoathiriwa na wanyama kwenye maeneo aliyoyataja kama Kipatimu, ni kweli Wizara yangu ina taarifa hizo na ndio maana nimesema kwamba kwenye eneo hilo na kwa kutambua matatizo haya tumepeleka huu mradi wa makusudi ambao mradi huu ni mkubwa sana, ambao unategemewa kuchukua muda wa miezi 72 na unatumia karibuni shilingi bilioni nne na nusu kwaajili ya kutoa elimu kwa wananchi wa eneo hilo.

Kwa hiyo, elimu watakayoipata wananchi hawa watakuwa na uwezo wa kujihami na matatizo madogo madogo yanayotokana na wanyamapori, lakini pia ikuweza kuwa na mawasiliano ya karibu na Wizara ili kukabiliana na matatizo hayo yanapojitokeza.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Matatizo yanayojitokeza kwa Mheshimiwa Mpanda, yako Pangani kwasababu tuna hifadhi ya Saadani na ndovu kuharibu mazao ya wananchi. Pamoja na utaratibu wa Serikali wa kulipa kifuta machozi cha shilingi laki moja na mabadiliko ya mara kwa mara ya Waheshimiwa Mawaziri katika Wizara hii: Je, Mheshimiwa waziri, kwa vile tena ni mpya katika Wizara hii uko tayari tena kupokea maombi ya wananchi wa Pangani ili yaweze kuharakishwa na kutatua tatizo hili?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, pamoja na mabadiliko ya mara kwa mara ambayo Mheshimiwa ameyasema kwamba yanatokea, nimhakikishie kwamba Wizara hazibadiliki na Serikali haibadiliki. Kwa hiyo, kumbukumbu zote zinazokuwepo tunazikuta. Matatizo ya ndovu Pangani tunayafahamu na mipango ya kutatua tatizo hilo iko mbioni. Kwa maana hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sio kwamba arudi nyuma kuwasilisha kwa mara nyingine tatizo hili, nimhakikishie tu kwamba tunalifahamu na mpango wa utatuzi unaendelea.

Na.15

**Utalii wa Kuzunguka Milima**

**MHE. WILLIAM H. SHELUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Utalii wa kuzunguka Mlima kwa kutembea au kwa magari unaziingizia fedha nyingi, nchi kama ya Shelisheli; na kwa kuwa, Tanzania ina maeneo mazuri ya milima kama vile Usambara yenye maua, miti, ndege wa kuvutia sana, na kadhalika:-

(a) Je, ni lini utalii wa aina hiyo utaanzishwa?

(b) Je, yale mashindano ya magari *(East Africa Safari Rally)* yaliyokuwa yakifanyika wakati wa Pasaka yataanza lini?

(c) Je, Serikali itakubali kutuma wataalam wa Utalii kwenda Shelisheli ili kujifunza aina hiyo ya utalii?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William Shelukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli utalii wa kuzunguka milima kwa kutembea kwa miguu au kwa magari unaziingizia fedha nchi nyingi duniani. Utalii wa kupanda milima kwa kutembea kwa miguu kwa kutumia njia maalumu upo na umeshamiri katika milima ya Kilimanjaro, Usambara, Pare, Oldonyolengai, Hanang, na milima ya Uluguru. Aina hii ya utalii huuzwa na wakala mbalimbali wa utalii ambao hupeleka wageni katika milima hiyo kulingana na matakwa ya wateja wao.

Aidha, utalii wa kuzunguka milima kwa magari bado haujaanzishwa. Hii ni kutokana na ukweli kuwa utalii wetu unasisitiza hifadhi ya mazingira, kwahiyo tumekuwa tukisisitiza zaidi utalii wa kupanda milima kwa miguu.

(b) Mheshimiwa Spika, mashindano ya magari, *East Africa Safari Rally*, yaliyokuwa yakifanyika hapo zamani wakati wa Pasaka yalikuwa yakiandaliwa na wakala kutoka Kenya kwa kushirikiana na chama cha *Automobile Association of Tanzania* yaani *(AAT)*.

Kutokana na kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977 ilipelekea pia ushirikiano wa mashindano haya kuvunjika na badala yake nchi ya Kenya ikaanzisha mashindano mengine yajulikanayo kama *Kenya Safari Rally* ambayo yanafanyika nchini humo tu.

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya 2000 nchi ya Kenya ilianzisha mashindano mengine zaidi ya yale ya *Kenya Safari Rally* yajulikanayo yajulikanyo kama *East Africa Classic* Safari *Rally*. Mashindano hayo yanajumuisha magari yaliyotengenezwa katika miaka ya 1974 kurudi nyuma na hufanyika kila baada ya miaka miwili mwezi Desemba.

Tangu kuanzishwa kwa mashindano hayo Tanzania imekuwa ikishiriki kwa kutegemea wafadhili.

Kwa mara ya mwisho mashindano yalifanyika Desemba, 2007 ambapo Watanzania wanne walishiriki. Mashindano hayo ambayo huanza na kumalizikia Mji wa Mombasa, kwa upande wa Tanzania yalianzia Gurdoto eneo la Momela kupitia njia za Sanya Juu, Himo, Usambara, Korogwe, Horohoro na kwenda Mombasa.

Kufuatana na maelezo hayo, uwezekano wa kuanzisha mashindano haya tena unategemea kuwepo kwa utashi wa wadau wa michezo ya aina hii hasa sekta binafsi kwa kushirikiana na *Automobile Association of* Tanzania kama ilivyo kwa vyama vingine vya michezo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Wizara yangu sio mdau wa moja kwa moja wa michezo, hata hivyo haina pingamizi ya kuanzishwa kwa mashindano haya endapo wadau kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo wataona inafaa kufanya hivyo.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali haina pingamizi kupeleka wataalam wa Utalii kwenda Visiwa vya Shelisheli kujifunza aina ya Utalii wa kuzunguka milima kwa magari

kwani ni moja ya nchi zinazofanya vizuri katika Sekta ya Utalii. Wizara italifanyia kazi pendekezo hili la Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri nilikuwa napenda kuishauri Serikali kwamba hili suala la mazingira twende nalo kimaendeleo kwa sababu usije ukatumia kigezo cha hifadhi ya mazingira kuchelewesha au kuzuia maendeleo. Ninavyoamini mimi ni kwamba magari ya kuzunguka hayaendi kwa *speed* kubwa yanakwenda kwa *speed* ndogo na yanatumia barabara zilezile zinazotumiwa na magari mengine kama hizi *Rally. N*adhani ni muhimu likatizamwa vizuri hili suala kwa sababu ni suala la kimaendeleo, lingesaidia kuboresha barabara ndogo za vijijini.

Swali la pili, kama mashindano haya yanayoendeshwa kwa mfano haya ya mwaka wa jana mwezi Desemba ambayo niliyashuhudia kwenye Jimbo la Bumbuli kama yanaingiza mapato sio jambo bora kama mapato kidogo asilimia yangeweza kulipa kwenye Halmashauri za Wilaya ambazo barabara zake zinatumika wakati wa mashindano hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu maswali Mbunge napenda kwanza nimshukuru kwa mawazo ambayo ni mazuri ambayo anayaleta kwenye Wizara yetu. Katika kujibu swali lake, kwanza ningependa kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama tulivyosema katika jibu letu la msingi hasa kipengele (c) kwamba Wizara haina pingamizi lolote la kupeleka wataalam Shelisheli kwenda kujifunza aina hii ya utalii. Wazo hili tumelichukua kwa *seriousness* inayohitajika. Kwa hiyo,i tutalifanyia kazi na tunaamini kwamba baada ya kujifunza tutalinganisha kati ya mazingira tunayozungumzia na utalii wenyewe na kuangalia katika hivi vitu viwili kuliko kupoteza kimoja.

Mheshimiwa Spika, swali la pili amezungumzia kuhusu mgawanyo wa mapato yanayotokana na mashindano ya magari. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, mashindano hayo hayapo. Kwa maana hiyo, suala la kugawana mapato na lenyewe *automatically* halipo, labda yatakapoanzishwa mashindano yenyewe ndiyo jambo lenyewe litaweza kujadiliwa.

**SPIKA:** Ingawa muda rasmi wa kipindi hiki cha Maswali na Majibu umepita kidogo, lakini naomba nimruhusu Mheshimiwa Kimaro kwa sababu nafasi ya maswali ilibanwa tulivyoanza mwanzo kwa matukio yale mengine ya kuapisha na kadhalika.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona na kuniruhusu niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza. Katika Jimbo la Vunjo, utalii wa kupanda mlima tumeuzoea. Sasa tumekwenda hatua ya pili utalii wa kitamaduni, yaani *cultural tourism* na lengo ni kwamba ifikapo mwaka 2010 Jimbo liwe ni *tourist destination.* Je, Serikali iko tayari kushirikiana na mimi kwa kutoa ushauri na watalaam ili lengo hilo la Jimbo la Vunjo kuwa *tourist destination* 2015 lifikiwe?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa utalii wa utamaduni, yaani *cultural tourism* ni moja ya mkakati na malengo ambayo tunayo katika Wizara na kwa kweli ni moja ya ahadi ambazo Chama cha Mapinduzi kiliahidi katika ilani kwenye eneo la uendelezaji wa utalii. Kwa maana hiyo, mawazo ya kusaidia ufikiwaji wa lengo hilo yanapokelewa sana na kwa hivyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara yangu ipo tayari kushirikiana naye. Tutaomba tuzungumze na watalaam wetu pamoja na yeye mwenyewe tuweze kushirikiana na pengine mawazo mazuri aliyonayo yasiishie tu Jimbo la Vunjo lakini pia yatusaidie kwenye maeneo mengine ya nchi yetu ambayo kwenye hili eneo la *cultural tourism* tuko nyuma ingawa vivutio tunavyo vingi sana. Kwa hiyo, namkaribisha sana Mheshimiwa Mbunge tuweze kuzungumzia jambo hili.

**SPIKA:** Ahsante sana. Niseme tu kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri Maige umeanza vizuri. *(Makofi)*

**MHE: HASSAN RAJAB KHATIBU:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, kanuni!

**MHE. HASSAN RAJAB KHATIBU:** Kanuni 68(7).

**SPIKA:** Eeh, endelea.

**MHE. HASSAN RAJAB KHATIBU:** Mheshimiwa Spika, Bunge letu hili linaendeshwa kwa mujibu wa kanuni ndiyo inayotawala katika kusimamia shughuli zote za Bunge Bungeni. Hivi asubuhi wenzetu bahati mbaya upande mwingine wa upinzani wametoka wote na sababu kubwa wanasema muafaka unasuasua kama ulivyozungumza.

Mheshimiwa Spika, Bunge hili halina mambo ya muafaka, muafaka ni huko ndani ya vyama. Hapa nataka kupata mwongozo kwamba huu utaratibu haukwenda kinyume na taratibu ya kanuni yetu ya Bunge? Kama umekwenda kinyume na kanuni za Bunge: Je, Bunge inachukua hatua gani dhidi ya utaratibu huu ambao walifanya wenzetu? Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuwe na subira. Jambo hili limetokea asubuhi ,sasa hivi na kwa maana fulani bado nitaendelea kupata maelezo kutoka kwa kiongozi wa upinzani, analihusisha vipi Bunge na suala hili. Lakini ninavyohisi ni kwamba, kwa kuwa jambo hili ni jambo la umma na Bunge ni mahali ambapo mambo ya umma yanaonekana waziwazi, pengine wenzetu wameona waonyeshe hapa nchini na kwingine kote jinsi ambavyo wanaona shida kwamba suala hili halipati ufumbuzi wa haraka kama walivyotarajia. Lakini tutatoa taarifa zaidi baada ya kusikiliza hayo waliyokusudia ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha. Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza, hivi kuna kanuni gani inayomfanya kiongozi yeyote kuja nyumbani kwako kukufuata asubuhi badala ya kukusubiri wakati upo ofisini na kukueleza suala kama hili? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda anaulizia kitendo cha Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed,-Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, kunifuata nyumbani. Spika lazima apatikane na watu wote wakati wowote na mahali popote, kwa sababu ama sivyo itakuwa vigumu. Leo ningeshtuka sana kama nisingejua hata sababu, halafu Wabunge wa Kambi ya Upinzani wote kwa pamoja wanaondoka tu na mtakumbuka hakuna chochote kingine kilitokea ila tulikuwa tunakaribia sasa kuingia kipindi cha Maswali. Baada ya kuapishwa wenzetu, wao wakainuka na kutoka nje.

Kwa hiyo, mimi nadhani kitendo cha Kiongozi wa Upinzani kunitaarifu kabla, sio kitendo cha kulaaniwa, ni kitendo kizuri tu cha uungwana ingawa yaliyofuatia sasa sina hakika kama unaweza kuyaita ni ya kiungwana. Kwa sababu kawaida ya sisi Watanzania ni kujadiliana ili tuelewane na sio kuwekeana au kufanyiana vitendo ambavyo vinaonyesha kukasirishwa na kuondoka mahali kwa sababu mjadala ndiyo utamaliza kila kitu pamoja na hilo ambalo wao wanasema haliendi vizuri litamalizika kwa mjadala tu na sio kwa ghadhabu. Ahsante sana.

Kama nilivyosema, Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha, sasa ni matangazo tu. Kwanza, kuhusu maswali nilikuwa naomba niwapeleke kwenye Kanuni yetu ya 39(10), inasema kwamba, maswali yatajibiwa Bungeni kwa mdomo, lakini endapo Mbunge mwenye swali hayupo Bungeni kuuliza swali lake na Spika hakutoa ruhusa kwa swali hilo kuulizwa na Mbunge mwingine. Basi Waziri aliyeulizwa swali atapeleka kwa Katibu jibu la maandishi naye Katibu ataliingiza jibu hilo kwenye taarifa rasmi.

Kwa hiyo, hawa wenzetu walioondoka wasilete tena hayo maswali yao kwenye mkutano huu kwa sababu kwa mujibu wa kanuni hii ni kwamba wamejivua wao wenyewe kuweza kuyauliza ila tu majibu kwa ajili ya *Hansard* yatawekwa kwa maandishi kwa mujibu wa Kanuni ya 30(10).

## MASWALI YALIYOJIBIWA KWA MAANDISHI

Na. 7

### Mpango wa Kupanua Barabara

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 1997 Serikali katika mpango wake wa kupanua barabara iliwavunjia wakazi wa maeneo ya Kimara nyumba zao na kuthaminisha nyumba hizo kwa lengo la kuwalipa waathirika kupitia maelezo ya Kamishna wa Ardhi na Maendeleo

ya Makazi katika Gazeti la Heko la Alhamisi, tarehe 25 Machi, 1999 kuhusu fidia kwa wenye hatimiliki, yenye Kumbukumbu namba MLHSD/1.140/33/143; na kwa kuwa kumekuwa na malalamiko kutoka kwa waathirika wa zoezi hilo hasa kwa kutokulipwa fidia kama ilivyoahidiwa:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kilichofidiwa na ni watu wangapi waliolipwa?

(b) Je, kuna malipo yoyote yaliyofanywa kwa Ndugu Charles Ladslaus Rweyemamu, mwenye hati Namba 64264, Kitalu cha Mitoma – Kimara Dar es Salaam iliyotolewa tarehe 1 Oktoba, 1983.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee (Viti Maalum) lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hakuna fedha zilizolipwa kwa ajili ya fidia kwa wananchi waliobomolewa nyumba zao ili kupisha upanuzi wa barabara mwaka 1997, eneo la Kimara Jijini Dar es Salaam na iliyokuwa Wizara ya Ujenzi. Hii ilitokana na ukweli kuwa, baada ya kufanya uchambuzi wa kina, ilibainika kuwa, maeneo hayo yalikwisha kufanyiwa uthamini na wahusika walikwishalipwa fidia mwaka 1972. Waathirika hao walikuwa kwenye makundi yafuatayo:-

(i) Walikuwepo wananchi ambao walikwisha kulipwa fidia mwaka 1972 lakini walibakia kwenye eneo hilo;

(ii) Walikuwemo wananchi waliouziwa maeneo hayo na wananchi waliokuwa wamelipwa fidia, ambapo wananchi hao waliyaendeleza bila ya kufahamu;

(iii) Walikuwemo wananchi waliovamia na kuishi kwenye maeneo hayo bila kumilikishwa kisheria; na

(iv) Waliokuwemo wananchi waliouziwa na wananchi waliokuwa wamelipwa fidia, ambao wamejenga nyumba maeneo hayo, kisha wakayapima maeneo yao na kupewa hati.

Mheshimiwa Spika, msimamo wa Serikali kwa wananchi wanaojenga kwenye maeneo ya hifadhi za barabara na maeneo mengine ambayo yalikwisha kubainishwa kwa ajili ya huduma za jamii na kulipiwa fidia ni kwamba hawalipwi fidia.

Mheshimiwa Spika, hakuna malipo yaliyofanyika kwa Ndugu Charles Ladslaus Rweyemamu, aliyekuwa mmoja wa waathirika wa upanuzi wa Barabara ya Ubungo kwa kuwa Serikali haikubuni upimaji wa viwanja hivyo, isipokuwa mwananchi huyo ni mmoja wa waliofanya juhudi binafasi za kujipimia eneo. Hali hii ilikuwa batili kisheria, kwa sababu eneo hilo halikuwa limepimwa viwanja kwa kuwa lilikuwa ni hifadhi ya barabara *(Road Reserve).*

Hata hivyo, wananchi wote walioathirika na upanuzi wa barabara hiyo, walimilikishwa viwanja katika eneo la Mbweni Malindi mwaka 1999, bila kulipia gharama halisi.

Na. 9

**Mradi wa Maendeleo wa Ziwa Tanganyika**

**MHE. KABWE Z. ZITTO** aliuliza:-

Kwa kuwa Mradi wa Maendeleo wa Ziwa Tanganyika unaohusisha nchi za Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Burundi ulipaswa uwe umeanza sasa, lakini hakuna taarifa zozote za Maendeleo ya mradi huo ambao uko chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais licha ya kwamba ungeweza kuleta Maendeleo makubwa kwa jamii ya wavuvi wa mwambao wa Ziwa Tanganyika na pia ungesaidia uanzishwaji wa viwanda vya kusindika samaki katika Mji wa Kigoma:-

(a) Je, ni nini tatizo la utekelezaji wa mradi huo?

(b) Je, ni lini Asasi za Kijamii za Mialo zitaanza katika Vijiji vya Mtanga, Kilalangabo, Mwamgongo, Kiziba, Zashe na Kagunga ili wavuvi wa Kigoma nao wafaidike na miradi ya uvuvi wa kisasa?

(c) Je, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi imeweka mikakati gani ya kuwavutia wawekezaji wa viwanda vya kusindika samaki na dagaa kutoka Ziwa Tanganyika ili kukuza uchumi wa mkoa na kuongeza ajira kwa vijana hasa ikizingatiwa kuwa tayari kuna mradi wa umeme wa Mto Malagarasi kupitia MCC ambao utaondoa kabisa kikwazo cha umeme katika uendelezaji wa viwanda Mkoani Kigoma?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Programu ya Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika, inahusisha nchi za Tanzania, Burundi, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Ili Programu iweze kutekelezwa, nchi husika inapaswa kuridhia Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika. Programu hii itahusisha miradi mitatu ambayo ni Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika, wenye gharama za Dola za Kimarekani 2.2 milioni ambazo ni msaada wa Mfuko wa Mazingira wa Dunia *(Global Environmental Facility)*, Mradi wa Uendelezaji wa Uvuvi Katika Ziwa Tanganyika wenye gharama za Dola za Kimarekani 7.4 milioni, ambazo ni Mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika na Mradi wa Udhibiti wa Maji Machafu katika Mji wa Kigoma – Ujiji, wenye gharama za *EURO* 6.0 milioni ambazo ni mkopo kutoka *NORDIC Fund.*

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya utekelezaji wa programu hii yalikwisha kukamilika, hata hivyo, utekelezaji haukuanza kama ilivyotarajiwa kutokana na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kuchelewa kuridhia Mkataba nilioutaja. Kutokana na juhudi za Mheshimiwa Rais wetu, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, imeweza kuridhia Mkataba huo mwezi Januari, 2008. Hatua inayofuatia ni kufanyika kwa kikao cha pili cha Mawaziri wa Mazingira wa nchi zote, ambacho kinatarajiwa kufanyika Bujumbura, Burundi, tarehe 24 Aprili, 2008, kwa lengo la kukamilisha masharti ya Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB).* Tunatarajia kuwa, utekelezaji wa mradi utaanza baada ya kukamilika kwa hatua hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003, inatambua Asasi za Kijamii katika mialo ya maeneo ya uvuvi nchini. Hivyo, Serikali imeweka mikakati ya kuanzisha asasi za namna hiyo katika maeneo ya uvuvi nchini na hadi sasa jumla ya vikundi 506 vya ulinzi wa rasilimali *(Beach Management Units – BMUs)* vimeanzishwa. Utaratibu wa kuanzisha vikundi kama hivi katika maeneo yote ya uvuvi nchini, unaendelea kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa Asasi za Kijamii katika Ziwa Tanganyika ni mojawapo ya kazi ambazo zitatekelezwa chini ya Mradi wa Usimamizi na Uendelezaji wa Bonde la Ziwa Tanganyika. Chini ya utaratibu huo, jamii za wavuvi zitahamasishwa kuunda vikundi vya ulinzi, kupewa elimu ya usimamizi shirikishi wa rasilimali ya uvuvi na kuwajengea uwezo ili waweze kuboresha maisha yao na rasilimali ya uvuvi kama ilivyofanyika kwenye maeneo mengine niliyoyataja.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara yangu, inatambua umuhimu wa uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi nchini ikiwemo Ziwa Tanganyika, kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi na kuinua kipato kwa jamii. Serikali kupitia Tathmini ya Rasilimali ya Uvuvi *(Fisheries Master Plan),* iliyofanyika mwaka 2001/2002, iliainisha suala la uwekezaji mkubwa katika Ziwa hilo kama suala muhimu. Hata hivyo, kama ilivyo kwa sekta nyingine, uwekezaji katika sekta ya uvuvi, hufanywa na sekta binafsi.

Matumaini yangu ni kwamba, kutokana na upatikanaji wa umeme kutoka Mradi wa *Millenium Challenge Corporation (MCC),* katika Mkoa wa Kigoma aliouzungumzia Mheshimiwa Mbunge, tunatarajia pawepo na uwekezaji wa kutosha.

Wizara yangu itakuwa tayari kushirikiana na wawekezaji watakaojitokeza kuwekeza katika viwanda vya samaki pale itakapohitajika na itaendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji.

Na. 10

**Shughuli za Uvuvi Katika Ukanda wa Bahari**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED** aliuliza:-

(a) Je, Tanzania ina ukanda wa bahari wenye urefu wa kilomita ngapi, na ni vyombo vingapi vya ndani ya nchi na vya kigeni vimepewa leseni za uvuvi katika kipindi cha mwaka 2007/2008?

(b) Je, ni vyombo vingapi kati ya hivyo vinalipa mrabaha *(royalty)* kutokana na mauzo ya mazao ya bahari wakiwemo samaki?

(c) Je, ni vyombo vingapi vinavua Bahari Kuu na huvua tani ngapi kwa wastani kwa mwaka?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Tanzania ina ukanda wa pwani wenye urefu wa kilomita zipatazo 1,424 kuanzia Moa, Wilaya ya Mkinga Mkoa wa Tanga hadi Msimbati, Wilaya ya Mtwara Vijijini katika Mkoa wa Mtwara. Vilevile, Tanzania inalo eneo la maji ya bahari lipatalo kilomita za mraba 287,000. Eneo hili limegawanyika katika eneo la Maji ya Taifa *(Territorial Waters)*, lenye upana wa maili za majini *(nautical miles)* 12, lenye eneo kilomita za mraba 64,000, pamoja na Ukanda wa Uchumi wa Bahari *(Exclusive Economic Zone – EEZ)*, wenye upana wa maili za majini *(nautical miles)* 188, wenye eneo la kilomita za mraba 223,000.

Mheshimiwa Spika, uvuvi katika eneo la bahari umegawanyika katika uvuvi mdogo na uvuvi mkubwa. Kwa kuzingatia mgawanyo huo, utoaji wa leseni za vyombo vya uvuvi katika eneo la bahari, huzingatia urefu wa vyombo vya uvuvi. Chini ya utaratibu huo ambao ni wa kisheria, Halmashauri za Wilaya husika, hutoa leseni kuvua kwa vyombo vyenye urefu usiozidi mita 11 na Wizara hutoa leseni za kuvua kwa vyombo vyenye urefu usiopungua mita 11 na vile vinavyovua kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari.

Katika mwaka 2007, Wizara yangu ilitoa leseni za uvuvi wa kamba kwa vyombo 12 vya Ki-Tanzania. Kati ya hivyo, chombo kimoja kilipewa leseni ya kuvua katika Maji ya Kina Kirefu *(Deep Sea Prawns).* Aidha, katika kipindi hicho, Wizara ilitoa leseni za uvuvi kwa vyombo vya kigeni 66 kutoka nchi za nje *(Distant Nation Fishing Vessels)*, ambazo zilivua katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari. Nchi hizo ni Japan (25), Ufaransa (18), Seychelles (7), Hispania (15) na Taiwan (1). Vyombo hivyo hulenga kuvua zaidi samaki aina ya Tuna ama Jodari na jamii zake.

Kuanzia Januari, 2008 hadi sasa, Wizara yangu imetoa leseni 11 za kuvua katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari; leseni hizo zimetolewa kwa nchi za Japan (8) na Hispania (3). Kwa upande wa uvuvi wa samaki aina ya kamba, hakuna leseni iliyotolewa hadi sasa.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kawaida vyombo vinavyovua samaki aina ya kamba, hulipa ada ya leseni ya chombo na leseni ya kuvua. Ada za leseni hizi hutozwa kulingana na uzito wa chombo *(Gross Tonnage - GRT)* na iwapo mmiliki wa chombo ana kiwanda kilichopasishwa *(Approved Shore Based Fish Processing Establishment)* cha kuchakata mazao ya uvuvi.

Chombo cha uvuvi hakilipi mrabaha bali kamba wanaovuliwa na vyombo hivi na kuuzwa nje ya nchi, ndiyo hutozwa mrabaha *(royalty)* na kwa kuzingatia daraja. Kwa mwaka 2007, jumla ya vyombo 12 vilipewa leseni ya uvuvi wa kamba na Serikali ilikusanya jumla ya shilingi 154,113,098.30 kama mrabaha *(royalty)*, kutokana na kamba waliovuliwa na kuuzwa nje ya nchi.

Aidha, vyombo vya kigeni vinavyopewa leseni za kuvua kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari, hutozwa ada ya utambulisho wa Chombo *(Vessel Identification Mark)* ya Dola za Kimarekani 2,000 kwa chombo na ada ya leseni ya kuvua ambayo ni Dola za Kimarekani 3,000 kwa mwezi kwa chombo au Dola za Kimarekani 16,000 kwa chombo kwa miezi 12.

(c) Mheshimiwa Spika, idadi ya vyombo vinavyovua katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari, hutofautiana mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, kwa mwaka 2005 kulikuwa na vyombo 79, mwaka 2006 vyombo 93; kati ya hivyo vyombo 87 vilikuwa vya kigeni na vyombo 6 vilikuwa vya Kitanzania; na mwaka 2007 vilikuwa vyombo 66 vyote ni vya nje. Aidha, kama nilivyoeleza hapo awali, kwa mwaka huu, Wizara imetoa leseni 11 hadi sasa kwa vyombo vya nje. Kulingana na takwimu tulizonazo, kiasi cha samaki kinachovuliwa kutoka kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari ni wastani wa tani zipatazo 17,322 kwa mwaka, kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita na samaki hao huuzwa katika masoko ya nchi mbalimbali.

**SPIKA:** Wageni wetu kwa leo kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro kutoka Kiteto, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Manyara ndugu Ole-Mukusi naomba Mwenyekiti usimame pale ulipo. Pole sana kwa ile kazi ngumu, lakini hatimaye ikazaa matunda. Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Babati Mjini - Rev. Wilson Mtatu yule pale huko Manyara ni masuti tu; Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kiteto - Ndugu Abubakar Mrisho, yule pale! Asante sana.

Mke wa Mheshimiwa Nangoro, Mama Nangoro tafadhali naomba usimame! Yule pale nadhani sasa utatulia kidogo baada ya harakati za kampeni. Naomba wote waliomsindikiza Mheshimiwa Nangoro kutoka kule Kiteto na Mkoa wa Manyara pia, tafadhali msimame ili Wabunge waweze kuwaona. Ni pamoja na wale wa vazi rasmi la kimasai ambalo linatutambulisha vizuri Tanzania katika ulimwengu wa nje. Karibu sana na asante sana kwa kumsindikiza Mheshimiwa Nangoro, na hakika mtapata matunda ya utumishi kwa kumchagua. *(Makofi)*

Pia wageni wengine ni wa Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir aliyeapishwa hivi leo. Ni wageni 20. Wageni wa Mheshimiwa Kwegyir wamesita sita, niliambiwa

kwamba na mumewe pia yupo, ndiyo yule amenyosha mkono kule. Hebu punga mkono Waheshimiwa Wabunge wakuone! Ahsante.

Karibu sana na tunawapongeza kwa kumsindikiza Mheshimiwa Al-Shaymaa na hakika atatimiza wajibu wake vizuri, kwa sababu taarifa tunazopata kutoka huko alikokuwa huko akifanya kazi, alikuwa ni mfanyakazi wa mfano wa kuigwa. *(Makofi)*

Tanzia: Katibu wa Bunge la Kenya ameleta taarifa ifuatayo, naomba niisome. Katibu wa Bunge *Obituary:* "*I regret to inform you that the Clerk of the National Assembly Mr. Samwel Waweru Ndindiri (EBS) passed away on Thursday 3rd April, 2008 following an illness. The late Ndindiri will be remembered for being meticulous in his work, his humility and commitment to Parliament, an institution he saved with dedication for close to three decades. The National Assembly of Kenya and especially his colleagues will regretly miss his insight and will forever be indebted to his mess contribution to the development of the institution. Yours Sincerely; S. Njenga, for the Clerk of the National Assembly of Kenya*."

Nina hakika Kamati ya Nje Ulinzi na Usalama ni vizuri baadaye wakutane ili watutengeneze ujumbe wa maandishi ambao tunaweza kuwapelekea wenzetu jirani hapo Kenya kwa msiba huu.

Vikao Mheshimiwa William Shellukindo Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini ameniomba niwatangazie Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kuwa leo tarehe 8 mwezi huu wa Nne mwaka 2008 saa 8.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati ghorofa ya nne Ukumbi Na. 432.

Mheshimiwa Jenister Mhagama Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii ameniomba nitangaze kwamba wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo wakutane leo saa saba mchana katika Ukumbi Na. 231.

Kwa hiyo, Kamati ya Maendeleo wakutane kwa kikao muhimu sana cha kujadili Muswada wa Sheria ya Kudhibiti na Kusimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2008 na kikao hicho ni saa saba mchana Ukumbi Na. 231 leo mchana.

Waheshimiwa Wabunge, mtaona kwamba kutokana na sikukuu jana haikuwezekana kufanya briefing, pia haikuwezekana kuwepo vikao vya *caucus* za vyama, kwa hiyo, natangaza kwamba *briefing* tutafanya pale ukumbi wa Pius Msekwa saa 5.30 asubuhi ili kutoa nafasi kwa Waheshimiwa Wabunge muweze kupata chai na wengine pengine kutaka kubadili mavazi pengine kwa sababu *normally* kwenye *briefing* uwe katika vazi rasmi la kibunge.

Kwa hiyo, *caucus* ya Vyama vya Siasa wale walio tayari ni saa 10.00 imepangwa. Kwa maana hiyo, hatutakuwa na kikao hiki cha Bunge, yaani hakitaendelea saa 11.00 kutoa nafasi ya Vyama vya Siasa Wabunge wahusika kuweza kukutana. Ila tukitoka hapa naomba Kamati ya Uongozi tukutane kwa kazi mahususi ya kuweza kusikilizana ili kuweza kuwapata Wenyeviti watatu kwa mujibu wa kanuni mpya.

Leo hii Naibu Spika anauguliwa, hayupo, basi Mwenyezi Mungu ameniwezesha tu kuendelea. Lingetokea jambo lolote mngekuwa hamna kiongozi kwa sababu nimebaki peke yangu. Wenyeviti ndiyo watachaguliwa tutaleta majina ili muweze kuwachagua. Kwa hiyo, Kamati ya Uongozi saa 4.45 kwa kikao kifupi kabla hatujaingia kwenye *briefing* kule Ukumbi wa Pius Msekwa. Kamati ya Uongozi inakutana pale kwenye Ukumbi wa Spika mara baada ya shughuli hizi.

Mheshimiwa Ameir, Katibu wa Kamati ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, ameniomba nitangaze kwamba Kamati ya Uongozi ya CCM itakutane leo mara baada ya *briefing.* Kwa hiyo, tunavyotoka kwenye *briefing* Wajumbe wa Kamati ya Uongozi wa Bunge wa Chama cha Mapinduzi tufuatane twende mahali ambapo ni kawaida kwa mkutano mara baada ya *briefing*.

Mheshimiwa Mohamed Rajab, mwalimu msaidizi wa *Bunge Sports Club* ameomba niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge kwamba tutaanza mazoezi kwenye uwanja wa Jamhuri saa 12.00 asubuhi kesho. Anasisitiza kwamba utaratibu wa magari upo na kukumbusha Waheshimiwa Wabunge wote kwa msisitizo kwamba michezo kwa afya ni muhimu sana na kwa kuwa sasa najisikia goti limepona nadhani tangazo hili limekuja wakati muafaka.

Nitafanya jitihada mara moja moja kuungana nao kwa sababu madaktari wanasema mazoezi uanze taratibu huendi moja kwa moja tu. Kwa hiyo, mara mtakuwa mkiniona pale.

Mwisho, Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwashukuru wale wote wamekuwa wakinitumia salamu za pole kwa masahibu yanayonipata hivi sasa ya kusemwa semwa katika namna ambayo haipendezi. Namshukuru Mungu, napenda kuwahakikishia kwamba shughuli za kuliimarisha Bunge hili ili lizidi kuwa ni Bunge imara linalokidhi matarajio ya wananchi wa Tanzania, nitaendelea nalo kwa nguvu zote. Ninalo ombi moja tu kwa hawa wenzangu ambao wameamua kuingia siasa za kiwango cha chini, siasa za maji taka, *gutter politics.* iMimi sisumbuliwi sana na hilo kwa maana hiyo nimekwishatoa maelekezo kwa Katibu wa Bunge aandae taarifa ya malipo yangu yote tangu siku nimeapishwa na taarifa hiyo mtapewa Waheshimiwa Wabunge kabla ya mkutano huu kwisha. Itaeleza kila kitu kwa kujibu yale ambayo ni rasmi.

Yale mengine ya mahusiano ya jamii sio kazi ya Katibu wa Bunge ajibu, kwa hiyo, nataka tujibu ambayo yatakuwa wazi na kila mtu ataelewa utaratibu gani Spika anatumia kwa kulipwa fedha. Wengine kwa mfano, Spika hupewa yeye posho, lakini mambo ya safari za Spika yanapitia kwa Wasaidizi wake na hata marejesho yanapitia kwa wasaidizi wake. Ninachoomba Waheshimiwa Wabunge, na kupitia kwenu niwaombe hawa jamaa wanaofanya mambo haya kwamba, tafadhali wasiwashambulie watoto wangu kwa sababu watoto wangu wanatumiwa nao *message.* Binti yetu ambaye ameolewa ametumiwa *message* chafu sana. Kama kuna mtu aliyewaudhi ni mimi sasa mnishambulie tu mimi na nina uwezo kamili wa kujibu kila shambulizi. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo na kwa kuwa sasa shughuli za leo ndiyo zimefikia mwisho naomba kuahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 4.50 asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,*
*Tarehe 9 Aprili, 2008, Saa Tatu Asubuhi)*